UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Je, Ramadhan itaweka Taqwa katika Nyoyo zenu Kusimama kwa ajili ya Ukombozi wa Palestina?

**HABARI NA MAONI**
Ongezeko la Watu Sio Chanzo cha Umaskini Tanzania

**MATOLEO**
Mikopo Katika Urasilimali Hainyanyui Jamii

**JIBU LA SWALI**
Kuzungumza Neno la Haki kwa Sauti Kubwa



# Je, Ramadhan itaweka Taqwa katika Nyoyo zenu Kusimama kwa ajili ya Ukombozi wa Palestina?

Afisi ya Habari Kenya

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 10/1445 Jumatatu, 01 Ramadhan 1445 H 11/03/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Je, Ramadhan itaweka Taqwa katika Nyoyo zenu Kusimama kwa ajili ya Ukombozi wa Palestina?

Hizb ut Tahrir / Kenya kwa furaha, inawapongeza Waislamu nchini na kote duniani kwa ujumla kwa kuwasili kwa mwezi mtukufu wa Ramadhan. Tunapoingia katika mwezi huu wa rehema, msamaha na kukombolewa na Moto wa Jahannam, tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) atujaalie nguvu na afya ya kutekeleza amali adhimu ya saumu ambayo si wajibu tu bali ni moja ya nguzo tano za Uislamu.

Ramadhan hii inakuja huku ulimwengu ukishuhudia mgongano kati ya matakwa ya Umma wa Kiislamu ya kushikamana na Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina na matakwa ya ukafiri wa Magharibi. Umma umeonyesha uaminifu wake kwa Uislamu na unatamani kwa dhati ushindi wa Mwenyezi Mungu. Ulimwengu unashuhudia kufilisika kiakhlaqi kwa maadili ya Magharibi huku wakiunga mkono mashambulizi ya kikatili ya 'Israel' huko Gaza. Dola na vyombo vya habari vya Magharibi vinaonyesha rangi zao halisi za unafiki na ubaguzi wa rangi.

Cha kusikitisha ni kwamba, unyama unaofanywa na majeshi ya Kiyahudi dhidi ya ndugu zetu wa Gaza bado haujachemsha nyoyo wala mishipa ya viongozi wa Kiislamu na majeshi yao! Enyi viongozi! Je, saumu yenu itaweka taqwa katika nyoyo zenu na kukata mahusiano na umbile la Kiyahudi? Enyi majeshi, je Ramadhan itawapeni taqwa ya kuwapuuza watawala wenu waliomfanyia khiyana Mwenyezi Mungu, Mtume wake na waumini ili muanze kuandamana kwenda Palestina na kupigana na jeshi la Mayahudi?

Katika historia yote, Ramadhan imekuwa ni mwezi wa ukombozi na ushindi. Historia hii angavu kwa hakika itahuisha ushindi katika Vita vya Badr, Qadisiyyah na Ein Jalut. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) atukubalie amali zetu na aujaalie Ummah huu mlinzi na ngao Khilafah kwa njia ya Utume. Khilafah ambayo itakusanya majeshi ya Waislamu ili kuling'oa umbile uaji la Kiyahudi na kukomboa sio tu Palestina inayokaliwa kwa mabavu bali ardhi zote za Waislamu.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:
# Kampeni ya Kitengo cha Wanawake ya Ramadhan
# “Ramadhan ni Mwezi wa Ushindi”




Karibu Ramadhan, mwezi wa ushindi, mwezi wa bishara njema, mwezi wa kujadidishwa imani na kutakasa nyoyo, mwezi wa utiifu na kushindana katika mambo mema. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyetufikisha Ramadhan, mwezi huu mtukufu ambao tunahisi ndani yake maana ya rehema na umoja baina ya Waislamu. Karibu, Ramadhan.

Je, Ramadhan ni mwezi wa ushindi kwa Waislamu wa Gaza, mwezi wa ushindi kwa Waislamu wa Palestina?

Ushindi kwa wale wote walio imara na kushikamana na ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na bishara njema ya Mtume wake (saw), katika nchi za Syria, Sudan, Myanmar, Kashmir, Turkestan Mashariki, India na duniani kote.

Katika kipindi cha miaka mia moja iliyopita, Umma wa Kiislamu umepoteza maisha na mali zisizohesabika, umekumbwa na maafa, umeshuhudia vita vya kikatili, na kuzuiwa kutekeleza ibada zake za kidini, zikiwemo saumu, swala na mavazi ya Kiislamu.

Lakini haukujisalimisha au kushindwa kwa sababu Umma huu lazima uwe na ushindi. Ndio maana unawaona makafiri wanakimbilia kwenye chinjachinja na mauaji ya halaiki na hata kutaka kufutwa kwa mwezi wa Ramadhan kwa sababu wanauogopa, kwa sababu ni mwezi ambao Waislamu wako karibu na Mola wao, wakiitamani zaidi Pepo na neema zake, na kukumbusha zaidi historia, ufunguzi na ushindi walioupata mujahidina. Majaribio yote haya ya uoga ya makafiri yanathibitisha kuwa Ramadhan ni mwezi wa ushindi kwa Waislamu.

Kwa hivyo, lengo letu katika mwezi huu mtukufu lazima liwe kuunganisha safu za Waislamu, na sisi sote tuna imani na hakika kwamba ushindi unakuja, ulimwengu wote utashuhudia, na makafiri watapata fedheha ya kushindwa, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Sisi katika Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir, tunakualikeni kuungana nasi katika kuunganisha maana ya ushindi na ujumbe wake na kueneza bishara njema yake sambamba na mwezi wa Ramadhan, mwezi wa ushindi, ushindi unakuja pasi na budi, na hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu atatunusuru ikiwa tutamnusuru Yeye na kutembea kwenye njia ya haki ambayo kwayo wahyi ulishuka.

وَأُخْرَى تُحِبُّونَهَا نَصْرٌ مِّنَ اللهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ

**“Na kinginecho mkipendacho, nacho ni nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi ulio karibu! Na wabashirieni Waumini!”** [As-Saff: 13]

**Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Mikopo Katika Urasilimali Hainyanyui Jamii



Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِذَا تَدَايَنتُم بِدَيْنٍ إِلَىٰٓ أَجَلٍ مُّسَمًّى فَٱكْتُبُوهُ ۚ

**"Enyi mlio amini! Mnapo kopeshana deni kwa muda ulio wekwa, basi andikeni."** [Al-Baqarah: 282]

Hii inaonesha kwamba suala la kukopa linaruhusiwa katika sheria ya Kiislamu. Sambamba na kwamba mikopo ni halali kisheria katika Uislamu lakini mikopo kupitia nidhamu ya kiuchumi inayochipuza kutoka kwa mfumo wa kisekula wa kirasilimali imekuwa ikididimiza jamii, na hii ni kutokana na vikwazo na vipengele vigumu vilivopo katika mikopo hiyo.

Inaonekana mikopo katika kiwango cha kitaifa chini ya nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali ilianza kurasimishwa toka karne ya kumi na tisa na kushamiri katika karne ya ishirini hasa baada ya kuwapatia uhuru wa bendera nchi ambazo ni mashamba yao kupitia ukoloni.

Kwa hiyo mojawapo ya sababu inayofanya nchi zisinufaike na mikopo ambayo nchi zinakopeshana au nchi zinakopa katika mashirika ya kifedha ya kimataifa kama Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa, nk ni kuwa mikopo hiyo inatumiwa na wakopeshaji yaani nchi zilizoendelea kama njia moja wapo ya kuendeleza ukoloni mamboleo katika nchi masikini.

Mikopo hii inakuwa na masharti magumu, kwa mfano riba na riba kubwa, kupunguza matumizi ya serikali, kupunguza wafanyakazi, na mengineyo. Hali kama hii hupelekea nchi husika kuendelea kutegemea nchi kubwa kwani kila mwaka huongeza deni lake la nje. Mfano deni la Tanzania Machi 2023 limeongezeka hadi kufikia trilioni Tsh94.8 kutoka trilioni Tsh87 kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la takribani asilimia 9.
Licha ya kuwa Mabepari wanatumia mikopo kama njia yao ya kuendeleza ukoloni mamboleo katika nchi masikini. Jamii imechukua mikopo kama miradi yao ya

***Endelea... UK 5***

kujipatia kipato. Mbali na mabenki, miaka ya hivi karibuni hasa kuanzia miaka ya 2000 kumeibuka kampuni na taasisi ndogo ndogo ambazo nazo zimejikita katika kutoa huduma ya kukopesha watu. Kwa mfano vikoba, vyama vya ushirika, vyama vya kuweka na kukopa, vikundi vya kusaidiana na upatu, nk.

Sababu na lengo la kuanzishwa kwa taasisi na kampuni hizi ni kile kinachodaiwa eti ni kuwakwamua au kuwainua watu kiuchumi hasa wale watu wa hali ya chini, lakini kiuhalisia sivyo bali ni unyonyaji wa wazi kabisa. Mfano, taasisi hizi zinatoza fomu za kuomba mkopo kiasi cha kuanzia Tsh5000 na Tsh5000 ya kutembelewa na viongozi wa kampuni hizo kwa ajili ya kufanya tathmini ya uwezo wa mkopaji kulipa deni lake.

Asilimia kubwa ya wanaochukua mikopo hii midogo ya "kujikwamua" wengi wao ni watu wa hali ya chini kiuchumi kama vile wafanya biashara wadogo, wakulima wadogo na watumishi wa umma. Miongoni mwa sababu zinazofanya watu kukopa katika taasisi hizo ni pamoja na serikali kuruhusu taasisi na kampuni kama hizo kufanya kazi hiyo ya kukopesha watu. Kwani lau serikali ingezuia taasisi hizo basi zisingeweza kufanya kazi.

Pia hali ngumu za kimaisha na uchumi mbaya, ambapo kutokana na hali ya mbinyo wa kimaisha mtu anaona kimbilio pekee ni kuchukua mkopo ili kukidhi mahitaji yake akiwa na matumaini butu ya kulipa baadaye na mwishowe kuishia kufilisiwa mali zao.

Suala lingine ni urahisi wa upatikanaji wa mikopo hiyo. Kwani mbali na kuwepo taasisi na makampuni ambayo yanakopesha watu kwa riba. Pia wapo watu binafsi ambao wamejiingiza katika biashara hiyo ya ukopeshaji na uelewa mdogo wa watu juu ya athari mbaya ya mikopo hii yenye riba, mara nyingi kutokana na hali ngumu ya kimaisha mtu huwa kama mfa maji kwa kuhangaika kiasi kwamba atashika popote ili mradi kuokoa maisha yake kwanza. Hivyo taasisi zinazokopesha huchukulia udhaifu huu kuwapa watu mikopo bila kujali athari zake mbaya.
Ama sababu nyingine ni mishahara isiyotosheleza kwa watumishi wa umma katika mahitaji yao hasa hasa makazi yao binafsi hali ambayo huwapelekea kuchukua mikopo ili kukidhi mahitaji yao ikiwemo kujenga, kusomesha nk. Hii ni kwa sababu wengi katika watumishi wa umma hukosa namna nyingine ya kuzalisha kipato chao kwani muda mwingi humaliza wakitumikia ajira zao.

Kuhusu suala hili la mikopo, jamii ni lazima itambue kwamba chanzo cha hali ngumu za maisha na matatizo yote ulimwenguni ni mfumo muovu wa kisekula wa kirasilimali ambao unawapa fursa hizi taasisi na makampuni na hata mtu mmoja mmoja kukopesha watu kwa riba. Hivyo ni wakati sasa jamii kufanya kazi usiku na mchana kuuondosha mfumo huu wa kiuchumi wa kinyonyaji na kisha kurejesha maisha ya Kiislamu ambapo uadilifu utatendeka, pia Uislamu utaondosha na kupiga marufuku taasis zote zinazojihusisha na mikopo ya riba kwani itkadi (aqeedah) ya Kiislamu ipo kinyume na riba na imekemea vikali swala la riba kama alivyosema Mwenyezi Mungu (swt):
**"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na acheni riba zilizo bakia, ikiwa nyinyi ni Waumini."** [Al-Baqara: 278]


Uislamu iwapo utatabikishwa kikamilifu kupitia serikali yake ya Khilafah utasimamia madeni kwa wenye kukopa na kukopesha kwa haki na uadilifu. Uislamu umeamrisha madeni yaandikwe iwe ni deni kubwa au deni dogo liandikwe kwa uadilifu bila kupunguza wala kuongeza chochote katika deni na katika maandishi.

Si hivyo tu, bali Uislamu unawajenga watu wake katika uchamungu na huruma kiasi kwamba hata pindi mtu anapomkopesha mwenzake, na mdaiwa akashindwa kulipa kwa wakati kutokana na changamoto za kimaisha, basi Uislamu umewaelekeza watu wake kuwa na subira kwa wadeni wao, pale Mwenyezi Mungu (swt) aliposema:
**"Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike. Na mkiifanya deni kuwa ni sadaka, basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua."** [Al-Baqara: 280]

Hii inaonesha ni kwa namna gani Uislamu upo kwa ajili ya maslahi ya watu kwa vile ni dini na mfumo uliotoka kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai. Kinyume na urasilimali ambao unawajenga watu wake katika hali ya maslahi tu, bila kujali madhara na uharibifu unaoweza kutokea kutokana na jambo fulani mfano hili la mikopo ya dhuluma na ulaghai inayowafanya watu kuwa kama wendawazimu.

**Ramadhani Njera**
**Mwanachama wa Hizb ut Tahrir Tanzania**

# HABARI NA MAONI
# Ongezeko la Watu Sio Chanzo cha Umaskini Tanzania



**Habari:**

Mnamo tarehe 12/03/2024, wakati wa uzinduzi wa toleo la 20 la Taarifa ya Hali ya Sasa ya Uchumi wa Tanzania jijini Dar es Salaam, Benki ya Dunia ilidai kuwa eti kasi ya ongezeko la watu inasababisha kudorora ukuaji wa uchumi nchini. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, wakati uchumi unatarajiwa kukua kwa 5.6 % hadi 6.0% mwaka 2024, Watanzania wengi bado wapo kwenye umaskini.

**Maoni:**

Dhana ya Ubepari kwamba ukuaji wa idadi ya watu unasababisha maendeleo duni ya kiuchumi ni matokeo ya nadharia za kiuchumi za "uhaba wa rasilimali" na "mahitaji ya binadamu yasiyo na kikomo". Mawazo hayo yalinasibishwa na idadi ya watu mwishoni mwa miaka ya 1700's na mwanzoni mwa miaka ya 1800's ambapo Mabepari walidai kuwa ongezeko la watu linasababisha viwango duni vya maisha.

Nadharia za Ubepari zinadai kwamba, kwa kuwa kuna kiwango maalumu cha rasilimali, ongezeko la watu hatimaye litapunguza mgawanyo wa kiasi cha rasilimali ambazo kila mtu anaweza kutumia, matokeo yake ni kusababisha uhaba mkubwa na umaskini. Kukabiliana na hili walipendekeza kuweka 'kizuizi cha kimaadili' (kujizuia kuwa na watoto 'wengi').

Kiuhalisia, Tanzania na nchi za Afrika kwa ujumla, zina rasilimali nyingi zikiwemo rasilimali watu ambazo zinaweza kabisa kuwafanya wawe na maendeleo kama si unyonyaji wa kikoloni wa mataifa ya kibepari. Kwa mfano, Tanzania inakadiriwa kuwa na mrundo wa kiwango cha dhahabu ya takribani wakia milioni 45 (tani 1,275), inachimba almasi kwa karne nyingi, mbali na madini mengine, kuna kilomita 1,424 ukanda wa pwani, hekta milioni 44 za ardhi ya kilimo na wastani wa hekta milioni 29.4 zinazofaa kilimo cha umwagiliaji, eneo la maji safi linakadiriwa kuwa kilomita za mraba 54,337, ambayo ni karibu asilimia 6.1 ya eneo lote la nchi, eneo la bahari ya kilomita za mraba 64,000, zaidi ya futi za ujazo trilioni 54 za gesi asilia nk.

Nadharia inayotokana na Malthus (ya kupunguza idadi ya watu) haina uhalisia, kwani tunachoshuhudia leo ni matumizi yasiyoisha ya rasilimali nyingi zinazosaidia idadi ya watu inayoongezeka. Wafuasi wa nadharia hii hawakuona wala kuzingatia maendeleo ya kiteknolojia ambayo yameongeza tija na kupunguza idadi ya magonjwa ya kuambukiza, na kufanya maisha kuwa yenye ufanisi. Leo mbinu za kisasa za kilimo zimepelekea uzalishaji wa chakula kuongezeka kwa kasi zaidi kuliko vile akina Malthus walivyotarajia. Ukuaji wa aina yake wa uchumi wa nchi za Asia kama China na India leo umewezeshwa sana na idadi yao kubwa ya watu.

Kwa hakika, kinachoifanya Tanzania na nchi nyingine zinazoendelea kuwa maskini, ni mfumo wa Ubepari unaotumia ukoloni kama mbinu yake isiyobadilika ya kufikia lengo lake la kinyonyaji. Sera za kinyonyaji za kikoloni kama vile soko huria, kukimbiza wataalamu nje ya nchi na uchumi wa karatasi, zimeyafanya mataifa yanayoendelea kuwa mashamba ya mataifa ya kikoloni na kuyaacha mataifa haya katika mdororo wa kiuchumi na minyororo ya kiuchumi ya nchi za Magharibi.

Ni wazi kwamba mwanadamu anahitaji mfumo wa haki na uadilifu ambao ni Uislamu, kupitia dola yake ya Khilafah itamkomboa mwanadamu kwa ukamilifu kutokana na uovu, uchumi wa kinyonyaji hadi kwenye ustawi wa kweli wa dunia na Akhera.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

**JIBU LA SWALI**

# Kuzungumza Neno la Haki kwa Sauti Kubwa

**Swali:**

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakatuh

Nina swali:

Surah Yunus ayah 90: فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ **"na Firauni na askari wake wakawafuatia"** na Surat Taha ayah 78: فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ **"Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake"**

Je, hii ina maana kwamba amri ya mtawala na kitendo cha mtawala ni kitu kimoja, ili tunaseme kuwa kusimama kinyume na amri zake ni sawa na kusimama kinyume na matendo yake, tukimaanisha kwamba tunaseme neno la haki mbele ya polisi wake au wasaidizi wake, kama kuzungumza mbele yake? أَفْضَلُ الْجِهَادِ كَلِمَةُ حَقٍّ عِنْدَ سُلْطَانٍ جَائِرٍ **"Jihad bora ni kusema neno la haki mbele ya mtawala jeuri"**. Shukran.

Una haki ya kubadilisha mpangilio wa maneno wa swali hili, na Mwenyezi Mungu akulipe kheri.

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullahi Wa Barakatuh

Kwanza: kuhusiana na ayah mbili ulizozitaja katika swali hili, ambazo ni katika yale ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Surah Yunus, ayah 90:

وَجَاوَزْنَا بِبَنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ بَغْياً وَعَدْواً

**"Tukawavusha bahari Wana wa Israili, na Firauni na askari wake wakawafuatia kwa dhulma na uadui"**, na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema katika Surat Taha, ayah 78:

فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ فَغَشِيَهُمْ مِنَ الْيَمِّ مَا غَشِيَهُمْ **"Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake. Basi kiliwafudikiza humo baharini kilicho wafudikiza!"** Ni kana kwamba unabainisha tofauti katika maana inayotokana na matumizi ya herufi الواو na herufi الباء katika maneno (askari wake), kama anavyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aya ya kwanza: فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ **"na Firauni na askari wake wakawafuatia"**, huku Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema katika ayah ya pili:

فَأَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ **"Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake"**. Maana ya "akawafuata" ni kwamba aliwafuata na akawafikia, kwa mujibu wa yale yaliyotajwa katika vitabu vya Tafsiri.

Lakini ayah ya kwanza فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ **"Firauni na askari wake"**, Kwa mujibu wa lugha, inafahamika kuwa Firauni alikuwa miongoni mwa waliowafuata, ikimaanisha kuwa kumfuata Musa, amani iwe juu yake, na Wana wa Israili (Bani Israil) wanajumuisha Firauni, Mwenyezi Mungu amlaani, na alikuwa miongoni mwa watu wale waliowafuata na kuwafikia. Hii ni kwa sababu الواو katika neno (na askari wake) hapa inaashiria kushiriki, yaani kushiriki kwa Firauni na askari wake katika kuwatafuta Wana wa Israili (Bani Israil).

Ama ayah ya pili: فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ **"Firauni pamoja na majeshi yake"**. Inaweza kueleweka kutokana nayo kwa mujibu wa lugha kwamba Firauni alishiriki pamoja na askari wake na mwenzao katika kuwasaka, lakini pia inaweza kueleweka kutokana nayo kwa mujibu wa lugha kwamba Firauni hakushiriki pamoja na askari wake na hakutoka pamoja nao, bali alitafuta tu msaada kutoka kwao katika kuwasaka, na hiyo ni kwa sababu neno "ba" katika lugha linaonyesha uandamani na usaidizi. Kwa hiyo neno (pamoja na askari wake) katika ayah hiyo linaweza kutumika kama lugha ya kuambatana, ikimaanisha kwamba Firauni aliandamana na askari wake katika kuwafuata Bani Israil, na pia inaweza kuchukuliwa kuwa ni kutafuta msaada, **ikimaanisha inaweza kuwa alikuwa pamoja nao, na inaweza kuwa alitafuta msaada kutoka kwa askari wake ili kuwafuatilia bila ya kushiriki nao**, maana yake ni kwamba waliowafuata ni askari wa Firauni bila ya Firauni mwenyewe.

**Utambulisho wa mojawapo ya maana hizi mbili (usindikizaji au usaidizi) unadhihirika kutokana na mchanganyiko wa aya hizo mbili:**

Ayah ya kwanza ina maana moja katika lugha. Na ni kwamba Firauni, Mwenyezi Mungu amlaani, aliungana nao, yaani, masahaba zake, katika kumkamata Musa (as). Maana ya Aya ya pili yaelekea ni katika lugha ya kuambatanisha, maana yake alifuatana nao katika kumkamata Musa, amani iwe juu yake, na pia yawezekana aliomba msaada, maana yake aliomba msaada kwa askari wake ili kumkamata Musa (as) bila ya Firauni kuwafuata, Mwenyezi Mungu amlaani katika hilo. Kwa sababu maana ya Aya hizo mbili hazipingani, maana ya kuziunganisha Aya hizo mbili ni kwamba Firauni alikuwa na jeshi lake katika kumfuata Musa

***Endelea... UK 8***

(as). Yaani ءابلا katika “pamoja na askari wake” hapa inaashiria maana ya kuandamana, kumaanisha kwamba alikuwa na jeshi lake katika kumfuata Musa, amani iwe juu yake. Hii ni kuhusiana na maana ya Aya hizo mbili.

**Pili: Ama Hadithi tukufu** iliyotajwa katika swali hili, imepokewa na Al-Tirmidhi katika Sunan yake kutoka kwa Abu Said Al-Khudri kwamba Mtume (saw) amesema:

**إِنَّ مِنْ أَعْظَمِ الْجِهَادِ كَلِمَةَ عَدْلٍ عِنْدَ سُلْطَانٍ جَائِرٍ "Hakika, miongoni mwa Jihad kubwa ni kusema neno la haki mbele mtawala jeuri"**. Abu Issa amesema, na katika sura hii kutoka kwa Abu Umamah, na hii hadith hasan ghareeb kwa mtazamo wake. Imetajwa katika Al-Mu’jam Al-Kabir ya Al-Tabarani kutoka kwa Abu Umamah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

**أَحَبُّ الْجِهَادِ إِلَى اللهِ كَلِمَةُ حَقٍّ تُقَالُ لِإِمَامٍ جَائِرٍ “Jihad inayopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni kusema neno la kweli kwa Imam jeuri”**. Katika riwaya nyengine ya Al-Tabarani kutoka kwa Abu Umamah, kwamba mtu mmoja alisema katika Jamarat: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni jihad gani iliyo bora? Akasema:

**أَفْضَلُ الْجِهَادِ كَلِمَةُ حَقٍّ عِنْدَ سُلْطَانٍ جَائِرٍ “Jihad iliyo bora kabisa ni kusema neno la kweli mbele ya mtawala jeuri.”** Yafuatayo yametajwa katika kitabu cha Aoun Al-Ma'boud katika kuielezea Hadithi hii: [... Kutoka kwa Abu Said Al-Khudri, ambaye amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: Jihad bora kabisa. ni neno la uadilifu kwa mtawala dhalimu. Swahaba wa Awn al-Ma'boud alisema:

(Jihad iliyo bora kabisa): Yaani, mojawapo ya bora zaidi, kama inavyo thibitishwa katika riwaya ya Al-Tirmidhi: Hakika, miongoni mwa jihadi kubwa kabisa (Neno la uadilifu) Na katika riwaya ya Ibn Majah kuna neno haki, na linalokusudiwa na neno hilo ni lile linaloamrisha mema au kukataza maovu, sawa iwe ni neno au maana yake, maandishi na mfano wa hayo.

(Kwa mtawala jeuri): Yaani dhalimu. Hakika hii imekuwa ni jihad bora kabisa, kwa sababu anayepigana dhidi ya adui anasitasita baina ya matumaini na khofu, bila kujua atashinda au atashindwa.

Mwenye mamlaka amedhulumiwa mkononi mwake, hivyo iwapo atasema ukweli na kumuamrisha M’aruf (mema), amefichua uharibifu na analenga kuangamia yeye mwenyewe. Hii inakuwa aina bora ya jihad kwa ajili ya kuishinda hofu, kama Al-Khattabī na wengineo walivyosema. (Au mtawala dhalimu (Amiri)): Inaonekana kwamba ni shaka kutoka kwa msimulizi.].

Kutokana na Hadith hii tukufu inaweza kufahamika kwamba jihad iliyo bora zaidi ni kusema neno la ukweli mbele ya sultan dhalimu, sio mbele ya wafuasi wake. Kinachomaanishwa na sultan dhalimu ni mwana mtawala dhalimu, awe rais, mfalme, waziri mkuu, au gavana. Ni lazima awe na mamlaka na utawala ili upendeleo huu utolewe katika kusema ukweli mbele yake.

Lakini hii haimaanishi kwamba hakuna wema katika kusema neno la ukweli mbele ya wafuasi wa mtawala dhalimu. Kusema neno la kweli siku zote ni jambo la kheri na la jema. Hata hivyo, faida maalum ambayo Mtume (saw) aliitaja katika Hadith tunayozingatia ni upendeleo unaohusiana na mwenye mamlaka, yaani, mtawala mwenyewe. Kwa sababu ya umuhimu wa kusema neno la ukweli mbele yake na hatari, ujasiri, na nguvu inayohusika, kama baadhi ya wafasiri wa Hadith walivyotaja:

**[... Al-Khattabi amesema: Hakika hiyo ikawa ndio jihad bora kabisa; Kwa sababu anayepigana na adui husitasita baina ya matumaini na hofu, bila kujua atashinda au atashindwa. Mwenye mamlaka amedhulumiwa mkononi mwake, basi iwapo atasema kweli na akamuamrisha M'aruf (mema), amefichuliwa uharibifu, na amejiweka kwenye maangamivu, na hii imekuwa ni aina bora za jihad kwa ajili ya kuishinda hofu. Al-Muzher amesema: Lakini ilikuwa bora zaidi kwa sababu dhulma ya Sultan inamhusu kila mtu chini ya utawala wake, na ni umati mkubwa. Kwa hivyo, ikiwa atakataza dhulma, basi ataleta manufaa kwa watu wengi zaidi ya kumuua kafiri...]**.

Mazungumzo yote ni juu ya mtawala dhalimu mwenyewe, sio juu ya wafuasi wake, wasaidizi, na askari.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

17 Rajab Al-Khair 1445 H

Sawia na 29/01/2024 M